# شرح القواعد الأربع

## *Sharh al-Qawaa´id al-Arba´ah*

*[Ufafanuzi wa misingi mine]*


***Mwandishi:***

الإمام صالح بن فوزان الفوزان

Imaam Swaalih bin Fawzaan al-Fawzaan

***Tarjama:***

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

00. Dibaji ... 3
01. Ufunguo wa furaha ... 4
02. Haniyfiyyah ndio dini ya Ibraahiym ... 11
03. Lengo la Allaah kuwaumba viumbe ... 15
04. Shirki inayaharibu matendo yote ... 19
05. Msingi wa kwanza ... 21
05. Msingi wa pili ... 24
06. Aina mbili ya uombezi ... 27
07. Msingi wa tatu ... 29
08. Kuna waliokuwa wakiabudu jua na mwezi ... 33
09. Kuna waliokuwa wakiwaaabudu Malaika na Mitume ... 34
10. Kuna waliokuwa wakiwaabudu waja wema ... 36
11. Kuna waliokuwa wakiabudu mawe na miti ... 41
12. Ukhatari wa kuwa na ujinga juu ya Tawhiyd ... 44
13. Msingi wa nne ... 48
14. Hitimisho ... 51

# 00. Dibaji

Himdi zote anastahiki Allaah na swalah na salaam zimwendee Mtume wetu Muhammad, familia yake na Maswahabah zake.

Wa ba´d:

Huu ni upambanuzi wa "*al-Qawaa´id al-Arbaa´ah*" iliyoandikwa na Shaykh-ul-Islaam na Mujaddid Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) kwa vile nimeona kuwa hakuna yeyote aliyekipambanua hapo kabla, basi nikapendelea kukipambanua kwa kiasi cha nafasi na uwezo wangu.

Allaah anisamehe kwa yale nitayokuwa nimefanya upungufu.

بسم الله الرحمن الرحيم

## 01. Ufunguo wa furaha

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

*Ninamuomba Allaah Mkarimu, Mola wa ´Arshi Kubwa, Akuhifadhi duniani na Aakhirah na akufanye ni mbarikiwa popote utapokuwa. Vilevile akufanye kuwa ni miongoni mwa wale wanapopewa hushukuru, wanapopewa mtihani husubiri na wanapotenda dhambi huomba msamaha - hakika mambo haya matatu ndio ufunguo wa furaha.*

**MAELEZO**

Hii ni "al-Qawaa´id al-Arbaa´ah" [misingi mine] iliyoandikwa na Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah).

Ni kitabu cha kipekee ambacho huwa kinachapishwa pamoja na "Thalaathat-ul-Usuwl" kwa sababu ya haja kiwe kwenye mikono ya wanafunzi.

"Qawaa´id" ni wingi wa neno "Qaa´idah", likiwa na maana ya msingi ambao kwao hutoa mambo na matawi mengi."

Misingi hii mine aliyoitaja Shaykh (Rahimahu Allaah) ndani yake mna elimu kuhusu Tawhiyd na shirki.

Ni upi msingi katika Tawhiyd? Ni upi msingi katika shirki? Watu wengi wanachanganya mambo haya mawili. Wanachanganya maana ya Tawhiyd na kuuliza ni kitu gani. Wanachanganya hali kadhalika maana ya shirki na

kuuliza ni kitu gani. Kila mmoja anafasiri mambo haya mawili kwa mujibu wa matamanio yake.

Lililo la wajibu kwetu ni kuirudisha misingi yetu katika Qur-aan na Sunnah, ili msingi huu uwe salama, sahihi na uwe umechukuliwa kutoka katika Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hili khaswa katika mambo haya mawili makubwa; Tawhiyd na shirki.

Shaykh (Rahimahu Allaah) hakutaja misingi hii kutoka kwake mwenyewe au kutoka kwenye kichwa chake kama wanavyofanya wachanganyikiwaji wengi. Bali ameitoa misingi hii kutoka katika Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume wa Allaah  (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na historia yake.

Ukiitambua misingi hii na kuifahamu, itakusahilikia baada ya hapo ni aina ipi ya Tawhiyd ambayo Allaah amewatuma kwayo Mitume Wake na akateremsha vitabu Vyake. Vilevile utaitambua shirki ambayo Allaah ametahadharisha nayo na akabainisha ukhatari na madhara yake duniani na Aakhirah. Jambo hili ni muhimu sana. Hili ni lazima kwako zaidi kuliko kuzijua hukumu zinazohusiana na swalah, zakaah, ´ibaadah mbalimbali na mambo mengine ya dini. Hili ndilo jambo la kwanza na la msingi, kwa sababu si swalah, zakaah, swawm, hajj na ´ibaadah nyenginezo hazisihi iwapo hazitojengwa juu ya ´Aqiydah sahihi, jambo ambalo ni kumpwekesha Allaah (´Azza wa Jall) kwa kumuabudu Yeye peke yake.

Hakika (Rahimahu Allaah) ametangulizi misingi hii mine kwa utangulizi mkubwa. Ndani yake mna kumuombea du´aa mwanafunzi na kumzindua kwa yale atayosema pale aliposema:

*"Ninamuomba Allaah Mkarimu, Mola wa ´Arshi Kubwa, Akuhifadhi duniani na Aakhirah na akufanye ni mbarikiwa popote utapokuwa. Vilevile akufanye kuwa ni miongoni mwa wale wanapopewa hushukuru, wanapopewa mtihani husubiri na wanapotenda dhambi huomba msamaha - hakika mambo haya matatu ndio ufunguo wa furaha."*

Katika utangulizi huu mkubwa Shaykh (Rahimahu Allaah) anamuombea kila mwanafunzi ambaye anaisoma ´Aqiydah yake kwa ajili ya kuifikia haki na

kuepuka upotevu na shirki, kwa sababu mtu kama huyu ana thamani Allaah amlinde duniani na Aakhirah. Yule ambaye Allaah atamlinda duniani na Aakhirah, hatoguswa na yenye kumchukiza si hapa duniani wala huko Aakhirah. Amesema (Ta´ala):

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ آمَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ۖ وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ

**"Allaah ni mlinzi wa wale walioamini. Anawatoa kutoka katika viza na kuwaingiza katika nuru. Wale waliokufuru walinzi wao ni mashetani." (02:257)**

Allaah akikulinda, basi atakuondosha kutoka katika viza, kama vya shirki, kufuru, mashaka na viza vya upindaji, na kukuingiza katika nuru ya imani, elimu yenye manufaa na matendo mema:

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ مَوْلَى الَّذِينَ آمَنُوا وَأَنَّ الْكَافِرِينَ لَا مَوْلَىٰ لَهُمْ

**"Hivyo ni kwa kuwa Allaah ni mlinzi wa wale walioamini na kwamba makafiri hawana mlinzi." (47:11)**

Allaah akikulinda kwa ulinzi Wake, mafanikio Yake na uongofu Wake hapa duniani na huko Aakhirah, utafurahi furaha ambayo hutohisi mahuzuniko hata siku moja. Katika dunia hii atakulinda kwa uongofu, mafanikio na kupita juu ya mfumo ulio salama. Aakhirah atakulinda kwa kukuingiza kwenye Pepo Yake ambapo utakuja kudumu humo milele. Humo hutohisi khofu, kupatwa na maradhi, kuhisi mahuzuniko, kuzeeka wala kupatwa na yenye kuchukiza. Hivi ndivyo Allaah anavyomuhifadhi mja Wake muumini duniani na Aakhirah.

Amesema:

*"... na akufanye ni mbarikiwa popote utapokuwa... "*

Lengo kubwa ni Allaah kukufanya kuwa ni mwenye kubarikiwa popote utapokuwa. Allaah anakujaalia kuwa ni mwenye kubarikiwa katika maisha yako, riziki yako, elimu yako, kitendo chako na kizazi chako. Baraka

zinakuandama popote unapokuwa na kuelekea. Hii ni kheri kubwa kabisa na fadhila kutoka kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

Amesema:

*"... Vilevile akufanye kuwa ni miongoni mwa wale wanapopewa hushukuru... "*

Tofauti na yule anayekufuru na kujivuna pale anapopewa neema. Hakika watu wengi wanapotunukiwa neema wanaikufuru. Badala yake wanaikana na wanaitumia katika kusikokuwa kumtii Allaah (´Azza wa Jall). Hii bila ya shaka inakuwa ni sababu ya kuangamia kwao. Ama kuhusu yule mwenye kushukuru, Allaah humzidishia:

لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ

**"Mkishukuru Nitakuzidishieni." (14:07)**

Allaah (´Azza wa Jall) huwazidishia wale wenye kushukuru kutokana na fadhila na wema Wake. Kwa ajili hiyo ikiwa unataka kupewa neema zaidi, mshukuru Allaah (´Azza wa Jall), na kama unataka kuiondosha neema, ikufuru.

Amesema:

*"... wanapopewa mtihani husubiri... "*

Allaah (Jalla wa ´Alaa) huwapa mitihani waja Wake. Huwapa mtihani wa misiba, yenye kuchukiza na maadui katika makafiri na wanafiki. Katika mnasaba huu wanahitajia kuwa na subira, matumaini na na kutokatika moyo na huruma wa Allaah. Wanatakiwa kuwa na uthabiti katika dini yao na wasitikiswe na mitihani au wakajisalimisha nayo. Ni lazima kwao wawe imara katika dini yao na wastahamili zile tabu wanazokumbana nazo. Wasiwe kama wale ambao wanapopewa mtihani wanababaika, wanakasirika na wanakatika moyo na huruma wa Allaah (´Azza wa Jall). Haya yanapelekea mitihani juu ya mitihani mingine na majanga juu ya majanga mengine. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Allaah anapowapenda watu basi huwapa mtihani. Ambaye ataridhia, hupata radhi, na atayekasirika, hupatwa na khasira."[1]**

**"Mitume ndio watu wenye kutiwa kwenye mitihani mikali. Halafu wale wenye kufanana na wao halafu wale wenye kufanana na wao."[2]**

Mitume walipewa mitihani na vivyo hivyo wakweli, mashahidi na waja wa Allaah waumini. Allaah (Ta´ala) amesema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَعْبُدُ اللَّهَ عَلَىٰ حَرْفٍ

**"Miongoni mwa watu yuko yule anayemwabudu Allaah ukingoni... "**

Bi maana pembezoni.

فَإِنْ أَصَابَهُ خَيْرٌ اطْمَأَنَّ بِهِ ۖ وَإِنْ أَصَابَتْهُ فِتْنَةٌ انقَلَبَ عَلَىٰ وَجْهِهِ خَسِرَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةَ ۚ ذَٰلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ

**"... inapompata kheri, hupata matumaini kwayo, na anapofikwa na mitihani hugeuka nyuma juu ya uso wake; amekhasirika duniani na Aakhirah. Hiyo ndiyo khasara ya wazi." (22:11)**

Dunia hii sio makazi ya kuneemeka, anasa, ladha, kufurahi na kushinda. Mambo hayako hivo siku zote. Ni kitu Allaah hufanya waja wakakutana nacho. Maswahabah, ambao ni watu bora wa Ummah, walikutana na majaribio na mitihani yepi? Amesema (Ta´ala):

وَتِلْكَ الْأَيَّامُ نُدَاوِلُهَا بَيْنَ النَّاسِ

**"Na hizo ni siku Tunazizungusha zamu baina ya watu." (03:140)**

[1] at-Tirmidhiy (04/601) na Ibn Maajah (4031). at-Tirmidhiy amesema: "Hadiyth hii ni geni." Vilevile imepokelewa na Ahamd (04/428).

[2] at-Tirmidhiy (07/131), al-Haakim (01/41) na al-Bayhaqiy (03/372). at-Tirmidhiy amesema: "Hadiyth hii ni nzuri na Swahiyh."

Kwa hiyo mja anatakiwa kujipoza kwa kutambua kwamba sio yeye peke yake aliyepewa majaribio. Haya tayari yameshatangulia kuwakuta vipenzi wa Allaah. Kwa ajili hiyo anatakiwa kujipoza nafsi yake, kusubiri na kusubiria faraja kutoka kwa Allaah (Ta´ala) - mwisho mwema ni wa wale wamchao Allaah.

Amesema:

*"... wanapotenda dhambi huomba msamaha - hakika mambo haya matatu ndio ufunguo wa furaha."*

Ama yule ambaye anapotenda dhambi haombi msamaha na bali anaendelea kuzama katika dhambi, huyu ni mla khasara - na kinga inatafutwa kutoka kwa Allaah. Lakini mja muumini kila pale anapofanya dhambi, anakimbilia kuomba msamaha:

وَالَّذِينَ إِذَا فَعَلُوا فَاحِشَةً أَوْ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ ذَكَرُوا اللَّهَ فَاسْتَغْفَرُوا لِذُنُوبِهِمْ وَمَن يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا اللَّهُ

**"Na wale ambao wanapofanya machafu au wakajidhulumu nafsi zao, humdhukuru Allaah wakaomba maghfirah kwa madhambi yao - na nani anayesamehe madhambi isipokuwa Allaah?" (03:135)**

إِنَّمَا التَّوْبَةُ عَلَى اللَّهِ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السُّوءَ بِجَهَالَةٍ ثُمَّ يَتُوبُونَ مِن قَرِيبٍ

**"Hakika tawbah inayokubaliwa na Allaah ni ya wale wanaofanya uovu kwa ujahili kisha wakatubia haraka haraka." (04:17)**

Neno "ujahili" haina maana ya ujinga unaofahamika, kwa sababu mjinga haadhibiwi, bali ni kinyume cha "umaizi". Kila mwenye kumuasi Allaah ni mjinga ambaye yuko na umaizi pungufu, akili pungufu na uanaadamu mpungufu. Mtu anaweza kuwa mwanachuoni na wakati huo huo akawa ni mjinga kwa mtazamo mwingine na ni kwamba anakuwa hana umaizi na uimara katika mambo:

ثُمَّ يَتُوبُونَ مِن قَرِيبٍ

**"... kisha wakatubia haraka haraka." (04:17)**

Hii ina maana ya kwamba kila wanapofanya dhambi, wanatubia. Hakuna yeyote ambaye amekingwa na dhambi, lakini himdi zote ni za Allaah kuona amefungua milango ya tawbah. Kwa ajili hiyo mja kila pale anapokosea anatakiwa kukimbilia kutubia. Lakini endapo hatotubia na kutaka msamaha, hii ni alama ya kula khasara. Mtu huyu kuna khatari akakata tamaa na huruma wa Allaah au shaytwaan akamjia na kumwambia: "Wewe huna tawbah."

Mambo haya matatu ndio ufunguo wa furaha; anapopewa hushukuru, anapopewa mtihani husubiri na anapotenda dhambi anaomba msamaha. Atayenyimwa mambo haya, au kimoja wapo, huyu ni mla khasara.

## 02. Haniyfiyyah ndio dini ya Ibraahiym

*Tambua - Allaah akuogoze katika kumtii - ya kwamba Haniyfiyyah ni dini ya Ibraahiym, nayo ni kumuabudu Allaah peke yake hali ya kuwa ni mwenye kumtakasia Yeye dini. Amesema (Ta´ala):*

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

***"Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu." (51:56)***

**MAELEZO**

Tambua - Allaah akuogoze katika kumtii... "

Hii ni du´aa kutoka kwa Shaykh (Rahimahu Allaah) na namna hii inatakiwa kwa mwalimu amuombee du´aa mwanafunzi.

Kumtii Allaah maana yake ni kujisalimisha katika maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake.

*"... ya kwamba Haniyfiyyah ni dini ya Ibraahiym... "*

Allaah (Jalla wa ´Alaa) amemuamrisha Mtume Wake kufuata dini ya Ibraahiym. Amesema (Ta´ala):

ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَنِ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۖ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

**"Kisha Tukakufunulia *Wahy* kwamba ufuate mila safi kabisa na ya asli ya Ibraahim, na hakuwa miongoni mwa washirikina." (16:123)**

Haniyfiyyah ni upwekeshaji ambayo ndio dini ya Ibraahiym (´alayhis-Swalaatu was-Salaam). "Haniyf" ni yule mwenye kumuelekea Allaah na kuvipa mgongo vyengine vyote. Hii ndio maana ya "Haniyf"; ni yule mwenye kumuelekea Allaah kwa moyo wake, matendo yake, nia na makusudio. Vyote

atekelezewe Allaah. Upande mwingine amevipa mgongo vyengine vyote. Allaah ametuamrisha kufuata dini ya Ibraahiym:

وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ ۚ مِّلَّةَ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ

**"Hakukufanyieni ugumu wowote ule katika Dini. Mila [iliyo safi kabisa na ya asli] ya baba yenu Ibraahiym." (22:78)**

Dini ya Ibraahiym ni kumuabudu Allaah hali ya kumtakasia Yeye dini. Hii ndio Haniyfiyyah. Hakusema kumuabudu Allaah peke yake, pasi na *Ikhlaasw*. Hii ina maana ya kwamba unatakiwa kujiepusha na shirki, kwa sababu ´ibaadah ikichanganyika na shirki inabatilika. Hakukuwi ´ibaadah isipokuwa pale itapokuwa ni yenye kusalimika na shirki aina zote kubwa na ndogo. Amesema (Ta´ala):

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ

**"Hawakuamrishwa jengine isipokuwa wamwabudu Allaah kwa imani safi kabisa na ya asli hali ya kumtakasia Yeye dini." (98:05)**

"Haniyf" ni yule mwenye kuelekea kwa Allaah (´Azza wa Jall) kitakasifu.

Allaah kawaamrisha ´ibaadah hii viumbe wote. Amesema (Ta´ala):

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

**"Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu." (51:56)**

Maana ya ´ibaadah waniabudu Mimi peke yangu na si mwengine. Hekima ya kuumbwa viumbe ni wamuabudu Allaah (´Azza wa Jall). Kuna baadhi walijisalimisha na ambapo wengine hawakufanya hivo. Lakini hii ndio hekima ya kuumbwa. Anayemuabudu mwengine asiyekuwa Allaah, anaenda kinyume na hekima ya kuumbwa viumbe, na kadhalika anaenda kinyume na maumbile na Shari´ah.

Ibraahiym ndiye baba wa Mitume waliokuja baada yake. Wote ni katika kizazi chake. Ndio maana amesema (Jalla wa ´Alaa):

وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ

**"Tukajaalia katika dhuria wake Unabii na Kitabu." (29:27)**

Wajukuu wote wa Ibraahiym (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) ni wana wa Israaiyl isipokuwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni kutoka katika kizazi cha Ismaa´iyl. Kwa hivyo Mitume wote wanatokamana na Ibraahiym (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) ikiwa ni ikramu kwake. Allaah alimfanya kuwa ni kiongozi wa watu, bi maana kiigizo:

قَالَ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا

**"Akasema: "Hakika Mimi Nakufanya uwe ni kiigizo kwa watu."" (02:124)**

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً

**"Hakika Ibraahiym alikuwa ni kiigizo." (16:120)**

Bi maana kiigizo wa kuigwa. Haya Allaah amewaamrisha viumbe wote. Amesema (Ta´ala):

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

**"Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu." (51:56)**

Ibraahiym aliwaita watu kumuabudu Allaah (´Azza wa Jall), kama walivyofanya Mitume wengine wote. Mitume wote waliwaita watu kumuabudu Allaah peke yake na kutomuabudu mwengine. Amesema (Ta´ala):

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

**"Hakika Tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na Twaaghuut [kila chenye kuabudiwa asiyekuwa Allaah]."" (16:36)**

Kuhusu Shari´ah ambayo ni maamrisho, makatazo, ya halali na ya haramu, inatofautiana kwa kutofautiana kwa nyumati kwa mujibu wa haja na mahitajio yao. Allaah anaweka Shari´ah kisha baadae anaifuta kwa kuweka Shari´ah nyingine. Hali iliendelea kuwa hivo mpaka kulipokuja Shari´ah ya Uislamu ikafuta Shari´ah zengine zote. Shari´ah hii itaendelea kubaki mpaka Qiyaamah kisimame. Kuhusu msingi wa Mitume, ambao ni Tawhiyd, unabaki, haufutwi na wala haufuti. Dini yao ni moja ambayo ni Uislamu, maana yake ni kumtakasia, kumuabudu Allaah Pekee. Shari´ah zinaweza kutofautiana na kufutwa, lakini Tawhiyd na ´Aqiydah ni moja kuanzia kwa Aadam mpaka kwa Mtume wa mwisho. Wote walikuwa wakiita katika Tawhiyd na kumuabudu Allaah peke yake. Kumuabudu Allaah ni kutii maamrisho ya Shari´ah Yake. Shari´ah hii ikifutwa, ´ibaadah inakuwa kwa kutendea kazi yale yaliyofuta na kutendea kazi yale yaliyofutwa hayazingatiwi tena kuwa ni kumuabudu Allaah.

## 03. Lengo la Allaah kuwaumba viumbe

*Ukishajua kuwa Allaah amekuumba ili umuabudu Yeye, basi jua ya kwamba ´ibaadah haiitwi kuwa ni ´ibaadah, pasi na Tawhiyd. Kama jinsi kuswali hakuitwi kuswali, pasi na wudhuu´. Shirki ikichanganyika na ´ibaadah inabatilika kama jinsi wudhuu´ unavyobatilika unapoingiliwa na hadathi.*

**MAELEZO**

Bi maana ukishaitambua Aayah:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

**"Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu." (51:56)**

Wewe ni katika wanaadamu na hivyo inakugusa pia. Umejua kuwa Allaah hakukuumba pasi na malengo, kwa sababu ule na unywe, au kwa sababu uishi maisha haya na utangetange huku na kule. Hakukuumba kwa sababu ya mambo haya. Amekuumba ili umuabudu. Amekuumbia viumbe hivi ili vikuwepesishie kumuabudu Yeye, kwa sababu huwezi kuishi pasi navyo. Vilevile huwezi kumuabudu isipokuwa kwa vitu hivi. Allaah amekuwepesishia navyo, ili umuabudu, sio kwa ajili ufurahi navyo, wende huku na kule ukiwa na furaha, ufanye dhambi, ufanye matendo ya jinai na kula na kunywa kile unachotaka. Hivi ndivyo wanavyofanya wanyama. Mwanaadamu ameumbwa na Allaah (Jalla wa ´Alaa) kwa ajili ya lengo kubwa na hekima kubwa, nayo ni kumuabudu Allaah. Amesema (Ta´ala):

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

**"Na Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu."**

Allaah hakukuumba ili umruzuku au umkusanyie pesa. Hivi ndivyo wanavyofanyiana wanaadamu pindi wanapofanyiana kazi ili kukusanya mapato. Allaah ni mkwasi kwa haya. Allaah hawahitajii viumbe. Amesema:

مَا أُرِيدُ مِنْهُم مِّن رِّزْقٍ وَمَا أُرِيدُ أَن يُطْعِمُونِ

**"Sitaki kutoka kwao riziki yoyote na wala Sitaki wanilishe." (51:57)**

Allaah (Jalla wa ´Alaa) anawalisha wenye njaa na halishwi. Hahitajii chakula. Yeye (Jalla wa ´Alaa) ni mkwasi na wala hana haja ya ´ibaadah zako. Ufalme Wake haupungui kitu ukikufuru. Wewe ndiye mwenye haja Naye. Wewe ndiye mwenye haja ya ´ibaadah. Katika huruma Wake ni kuwa amekuamrisha kumuabudu. Ni kwa ajili ya maslahi yako. Ukimuabudu, basi (Subhaanahu wa Ta´ala) atakukirimu kwa malipo na thawabu. ´Ibaadah ni sababu ya Allaah kukukirimu duniani na Aakhirah. Hivyo basi, ni nani anayefaidika kwa ´ibaadah? Ambaye anafaidika kwa ´ibaadah ni mja Mwenyewe. Kuhusu Allaah (Jalla wa ´Alaa), Yeye amejitosheleza na waja Wake.

"... *basi jua ya kwamba ´ibaadah haiitwi kuwa ni ´ibaadah, pasi na Tawhiyd. Kama jinsi kuswali hakuitwi kuswali, pasi na wudhuu´.*"

Ukishatambua kuwa Allaah amekuumba ili umuabudu, basi kadhalika unatakiwa kujua kuwa ´ibaadah ambayo Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) anairidhia haiwi sahihi yenye kuridhiwa na Allaah mpaka itimize sharti mbili. Kukikosekana sharti moja wapo, inabatilika.

Sharti ya kwanza: Kitendo hicho awe ametekelezewa Allaah peke yake na kiwe kimetakasika na aina zote za shirki. Kikichanganyika na shirki, kinabatilika. Kwa mfano wudhuu´ unatenguka iwapo utachanganyika na hadathi. Vivyo hivyo ´ibaadah yako inabatilika ukimuabudu Allaah na baada ya hapo ukatumbukia katika shirki.

Sharti ya pili: Kumfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kila ´ibaadah ambayo hakuweka Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni batili na ni yenye kukataliwa na kwamba ni Bid´ah na ukhurafi. Kwa ajili hii amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Atakayefanya kitendo kisichoafikiana na amri yetu, atarudishiwa."[3]**

Katika upokezi mwingine imekuja:

**"Atakayezua katika amri yetu hii yasiyokuwemo, atarudishiwa."[4]**

´Ibaadah ni lazima iwe ni yenye kuafikiana na yale aliyokuja nayo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), sio na yale ambayo watu wanaonelea kuwa ni mazuri na nia na makusudio yao. Midhali hakisapotiwi na dalili kutoka katika Shari´ah, basi kitendo hicho ni Bid´ah isiyomfaa mwenye nayo. Uhakika wa mambo ni kuwa kinamdhuru kwa sababu ni maasi hata kama atadai kuwa anajikurubisha kwacho kwa Allaah (´Azza wa Jall).

Kwa hiyo ni lazima ´ibaadah itimize sharti mbili hizi ili iweze kuwa sahihi na yenye kumfaa mwenye nayo; *Ikhlaasw* na yenye kuafikiana na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ikichanganyika na shirki, inabatilika, na ikichanganyika na Bid´ah isiyokuwa na msingi, inabatilika pia. Hakuna faida ya ´ibaadah ikiwa haikutimiza sharti hizi mbili kwa sababu itakuwa inahusiana na kitu ambacho hakikuwekwa na Allaah (´Azza wa Jall) - na Allaah anakubali tu yale aliyoyaweka katika Kitabu Chake au kupitia Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Hakuna kiumbe yeyote ambaye ni wajibu kumfuata asiyekuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wengine wote wanafuatwa na kutiiwa kwa sababu tu wamemfuata na kumtii Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hata hivyo hawafuatwi ikiwa hawatomfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

[3] Muslim (1718).

[4] al-Bukhaariy (2697) na Muslim (1718)

أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ

**"Mtiini Allaah na mtiini Mtume na wale wenye madaraka katika nyinyi." (04:59)**

Wenye madaraka ni wale watawala na wanachuoni. Ni wajibu kuwatii endapo watamtii Allaah. Hata hivyo haitofaa kuwatii wala kuwafuata ikiwa wataenda kinyume na Allaah. Hakuna kiumbe yeyote ambaye anatakiwa kutiiwa kipekee isipokuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wengine wote wanatiiwa na kufuatwa wakimfuata na kumtii Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hii ndio ´ibaadah sahihi.

## 04. Shirki inayaharibu matendo yote

*Unapojua kuwa shirki inapoingia katika ´ibaadah inaiharibu na kubatilisha kitendo hicho na mwenye nayo anakuwa ni katika wadumishwaji Motoni milele, ndipo utaona kuwa suala hili ni muhimu sana kwa ulazima kulitambua. Huenda Allaah akakusalimisha na mtego huu, jambo ambalo ni kumshirikisha Allaah. Allaah (Ta´ala) amesema juu yake:*

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

***"Hakikaha hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa Amtakae." (04:116)***

*Hili litatambulika kwa kuijua misingi mitatu ambayo Allaah (Ta´ala) ameitaja katika Kitabu Chake:*

**MAELEZO**

Midhali umejua ni nini Tawhiyd, nayo ni kumpwekesha Allaah katika ´ibaadah, na lazima vilevile ujue shirki ni kitu gani. Kwa kuwa yule asiyekitambua kitu hutumbukia ndani yake. Ni lazima ujue aina mbalimbali za shirki ili uweze kuziepuka, kwa sababu Allaah ametahadharisha shirki na kusema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

**"Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa Amtakae." (04:48)**

Huu ndio ukhatari wa shirki ambao unaharamisha Pepo:

إِنَّهُ مَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ

**"Hakika mwenye kumshirikisha Allaah bila shaka Allaah atamharamishia Pepo." (05:72)**

Vilevile inaharamisha msamaha:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

**"Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa Amtakae." (04:48)**

Hii ni khatari iliokubwa, ambayo ni lazima uitambue, kabla ya kila kitu kingine, kwa sababu shirki wamepotea kwayo wenye fahamu na akili. Hebu wache tujue shirki ni kitu gani kwa mujibu wa Qur-aan na Sunnah. Allaah hakutahadharisha kitu isipokuwa amekibainisha na kadhalika hakuamrisha kitu isipokuwa amewabainishia nacho watu. Hakutahadharisha shirki na kuiacha hivo hivo kijumla. Uhakika wa mambo ni kuwa ameibainisha katika Qur-aan tukufu na vilevile Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameibainisha katika Sunnah kwa njia ya wazi kabisa. Hivyo tukitaka kujua shirki ni kitu gani, ni lazima turejee katika Qur-aan na Sunnah na sio katika maoni ya huyu na yule.

## 05. Msingi wa kwanza

*Msingi wa kwanza utambue kuwa makafiri ambao Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwapiga vita, walikuwa wakikubali ya kwamba Allaah (Ta´ala) ndiye Muumbaji Mwenye kuyaendesha mambo. Hata hivyo hili halikuwaingiza wao katika Uislamu. Dalili ya hilo ni Maneno Yake (Ta´ala):*

قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّن يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَارَ وَمَن يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَن يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ۚ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ ۚ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ

**"Sema: "Nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini au nani anayemiliki kusikia na kuona na nani anayemtoa [aliye] hai kutoka maiti na anayemtoa maiti kutoka [aliye] uhai na nani anayeendesha mambo? Watasema: "Ni Allaah". Basi sema: "Je basi hamchi?" (10:31)**

**MAELEZO**

Msingi wa kwanza utambue kuwa makafiri ambao Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwapiga vita, walikuwa wakikubali Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah. Pamoja na kukubali kwao Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah hakukuwafanya waingie katika Uislamu na hakukufanya damu na mali zao zisichukuliwe. Hili linafahamisha ya kwamba Tawhiyd haihusiani na kuthibitisha uola peke yake na vivyo hivyo shirki haihusiani tu na kuamini ya kwamba Allaah hakupwekeka katika matendo Yake. Uhakika wa mambo ni kwamba hakuna yeyote asiyeamini kuwa Allaah amepwekeka katika matendo Yake isipokuwa viumbe waovu na waliopinda peke yake. Vinginevyo ni kwamba viumbe wote wanathibitisha Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah. Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah maana yake ni kwamba Allaah peke yake ndiye muumbaji, mruzukaji, muhuishaji, mfishaji na mwenye kuendesha mambo. Kwa ibara nyingine iliyofupi Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah ni kumpwekesha Allaah katika matendo Yake.

Hakuna kiumbe yeyote aliyedai kuwa kuna yeyote anayeumba, anayeruzuku, anayehuisha au anayefisha pamoja na Allaah (Ta´ala). Washirikina walikuwa wakiamini kuwa Allaah peke yake ndiye muumbaji, mwenye kuruzuku, mwenye kuhuisha na kufisha:

وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ

**"Ukiwauliza: "Ni nani aliyeumba mbingu na ardhi?" bila shaka watasema: "Allaah." (31:25)**

قُلْ مَن رَّبُّ السَّمَاوَاتِ السَّبْعِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ سَيَقُولُونَ لِلَّهِ

**"Sema: "Nani Mola wa mbingu saba na Mola wa ´Arshi tukufu?" Watesema: "Ni ya Allaah Pekee." (23:86-87)**

Soma mwisho wa Suurah "al-Muu´minuun" uone namna ambavyo washirikina walikuwa wakithibitisha Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah. Kadhalika Suurah "Yuunus":

قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّن يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَارَ وَمَن يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَن يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ۚ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ ۚ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ

**"Sema: "Nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini au nani anayemiliki kusikia na kuona na nani anayemtoa [aliye] hai kutoka maiti na anayemtoa maiti kutoka [aliye] uhai na nani anayeendesha mambo? Watasema: "Ni Allaah". Basi sema: "Je basi hamchi?" (10:31)**

Walikuwa wakithibitisha haya pasi na shaka.

Tawhiyd haina maana kuwa ni kukiri Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah, kama wanavyodai wanafalsafa na watafiti katika ´Aqiydah zao. Wanaonelea kuwa Tawhiyd ni kuthibitisha kuwa Allaah peke yake ndiye muumbaji, mruzukaji, muhuishaji na mfishaji. Wanasema:

"Ni Mmoja katika dhati Yake na hagawanyiki, ni Mmoja katika sifa Zake na hafanani na yeyote na ni mmoja katika matendo Yake na hana mshirika."

Haya si chengine zaidi ya Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah. Hakuna kitabu chochote kilichoandikwa na wanafalsafa, isipokuwa mtaona kuwa hawaongelei jengine zaidi ya Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah. Hii sio aina ya Tawhiyd ambayo Allaah aliwatuma kwayo Mitume. Kuthibitisha hili peke yake halimnufaishi kitu mwenye nayo. Aina hii ilikuwa ikithibitishwa na washirikina na viongozi wa kikafiri na halikuwafanya wakatoka katika ukafiri wala kuwaingiza katika Uislamu. Hili ni kosa kubwa kabisa. Mwenye kuamini namna hii hakuzidisha kitu zaidi ya kile alichokuwa akiamini Abu Jahl na Abu Lahab.

Wanateolojia wa leo wanathibitisha tu aina ya Tawhiyd yenye kusema kuwa Allaah amepwekeka katika uola Wake, hawagusii kabisa aina ya Tawhiyd yenye kusema kuwa Allaah peke yake ndiye mwenye haki ya kuabudiwa. Kuita hii kuwa ndio Tawhiyd ni kosa kubwa kabisa.

Kuhusu shirki, wanaifasiri ifuatavyo:

"Mtu kuamini kuwa kuna ambaye anaumba au anaruzuku pamoja na Allaah."

Haya hayakusemwa si na Abu Jahl wala Abu Lahab. Hawakusema kuwa kuna ambaye anaumba wala kuruzuku pamoja na Allaah. Bali uhakika wa mambo ni kwamba walikuwa wakithibitisha kuwa Allaah ndiye mwenye kuumba, mwenye kuruzuku, mwenye kuhuisha na mwenye kufisha.

## 05. Msingi wa pili

*Msingi wa pili wanasema: "Sisi hatuwaombi wala hatuelekei kwao isipokuwa ni kwa sababu ya kutafuta ukurubisho na uombezi. Dalili ya ukurubisho ni maneno Yake (Ta´ala):*

وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ إِنَّ اللَّهَ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ فِي مَا هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ كَاذِبٌ كَفَّارٌ

***"Na wale wanaowafanya wengine badala Yake kuwa walinzi [wakisema]: "Hatuwaabudu isipokuwa kwa lengo la kutukurubisha kwa Allaah ukaribu." Hakika Allaah Atahukumu baina yao katika yale yote waliyokhitilafiana nayo. Hakika Allaah Hamwongoi aliye muongo, kafiri." (39:03)***

**MAELEZO**

Washirikina ambao Allaah amewaita kuwa ni "washirikina" na akawahukumu kudumu Motoni milele, hawakushirikisha katika uola wa Allaah, bali katika ´ibaadah. Hawasemi kuwa waungu wao wanaumba, wanaruzuku, wanadhuru au wanaendesha mambo pamoja na Allaah. Kazi yao ilikuwa ni kuwafanya tu kuwa waombezi. Allaah (Ta´ala) amesema:

وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَٰؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِندَ اللَّهِ

**"Na wanaabudu asiyekuwa Allaah ambao [hawawezi] kuwadhuru na wala kuwanufaisha na wanasema: "Hawa ni waombezi wetu mbele ya Allaah."" (10:18)**

Wanakubali kuwa hawadhuru na wala hawanufaishi na kwamba ni waombezi peke yao ambao wanamweleza Allaah mahitajio yao. Wanawachinjia na wanawawekea nadhiri. Hawakufanya haya kwa sababu wanaona kuwa wanaumba, wanaruzuku, wananufaisha na wanadhuru. Bali ni kwa sababu wanawaombea mbele ya Allaah - hii ndio dini ya washirikina.

Hii leo ukijadiliana na mwabudu kaburi atasema maneno haya haya:

"Mimi najua kuwa walii au mja huyu mwema hanufaishi wala hadhuru. Lakini ni mja mwema na ninachotaka kutoka kwake aniombee mbele ya Allaah."

Kuna uombezi ambao ni haki na ambao ni batili. Uombezi ambao ni haki na sahihi ni ule uliotimiza sharti mbili:

1- Uwe kwa idhini ya Allaah.

2- Yule anayeombewa awe ni katika wapwekeshaji, yaani katika watenda dhambi wapwekeshaji.

Kukikosekana sharti moja katika sharti hizi mbili, uombezi unakuwa batili. Amesema (Ta´ala):

مَن ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِندَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

**"Nani huyu ambaye anashufai mbele Yake bila ya idhini Yake." (02:255)**

وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنِ ارْتَضَىٰ

**"Na wala hawamuombei uombezi yeyote yule isipokuwa yule Anayemridhia." (21:28)**

Hawa wenye kuombewa ni watenda dhambi wapwekeshaji. Kuhusu makafiri na washirikina, hautowafaa kitu uombezi wa waombezi:

مَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ حَمِيمٍ وَلَا شَفِيعٍ يُطَاعُ

**"Madhalimu hawatokuwa na rafiki na wala mwombezi anayetiiwa." (40:18)**

Watu hawa wamesikia kunazungumzwa kuhusu uombezi na wala hawakujua maana yake. Kwa ajili hiyo ndio wakaanza kuwaomba maiti uombezi bila ya idhini ya Allaah (´Azza wa Jall). Wameuomba vilevile kutoka kwa washirikina ambao wao wenyewe hautowafaa kitu uombezi wa waombezi. Watu hawa ni

wajinga juu ya uombezi sahihi, kadhalika uombezi batili. Kwa hivyo uombezi una sharti na haukuachwa hivi hivi.

## 06. Aina mbili ya uombezi

*Dalili ya uombezi ni maneno Yake (Ta´ala):*

وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَٰؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِندَ اللَّهِ

***"Na wanaabudu asiyekuwa Allaah ambao [hawawezi] kuwadhuru na wala kuwanufaisha na wanasema: "Hawa ni waombezi wetu mbele ya Allaah." (10:18)***

*Kuna aina mbili za uombezi:*

*Aina ya kwanza:* *Uombezi wenye kukanushwa.*

*Aina ya pili:* *Uombezi wenye kuthibitishwa.*

*Uombezi wenye kukanushwa ni ule wenye kutafutwa kutoka kwa asiyekuwa Allaah katika yale yasiyoweza kufanya yeyote isipokuwa Allaah. Dalili ni maneno Yake (Ta´ala):*

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَنفِقُوا مِمَّا رَزَقْنَاكُم مِّن قَبْلِ أَن يَأْتِيَ يَوْمٌ لَّا بَيْعٌ فِيهِ وَلَا خُلَّةٌ وَلَا شَفَاعَةٌ ۗ وَالْكَافِرُونَ هُمُ الظَّالِمُونَ

***"Enyi mlioamini! Toeni katika Tulivyokuruzukuni kabla haijafika Siku ambayo hakutakuweko mapatano [ya fidya] humo wala urafiki wala uombezi. Na makafiri wao ndio madhalimu." (02:254)***

*Uombezi wenye kuthibitishwa ni ule wenye kutafutwa kutoka kwa Allaah na mwombezi amekirimiwa uombezi na muombewaji ni yule ambaye Allaah ameridhia maneno yake na vitendo vyake baada ya kupewa idhini. Amesema (Ta´ala):*

مَن ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِندَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

***"Nani huyu ambaye anashufai mbele Yake bila ya idhini Yake." (02:255)***

**MAELEZO**

Kuna aina mbili ya uombezi:

Aina ya kwanza ya uombezi ni ule ambao Allaah (Jalla wa ´Alaa) ameukanusha na ni ule uombezi unaokuwa pasi na idhini Yake (Subhaanahu wa Ta´ala). Hakuna yeyote awezae kushufaia mbele ya Allaah isipokuwa kwa idhini Yake. Pindi kiumbe bora kabisa na Mtume wa mwisho Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) atapotaka kuwaombea watu siku ya Qiyaamah, ataanguka hali ya kusujudu mbele ya Mola Wake, amuombe, amtape na kumsifu mpaka pale atapoambiwa:

**"Nyanyua kichwa chako. Zungumza utasikizwa, omba utapewa."**[5]

Hatoombea isipokuwa baada ya idhini Yake.

Aina ya pili ya uombezi wenye kuthibitishwa ni ule unaokuwa kwa wale wenye kumuabudu Allaah peke yake. Mshirikina hautomfaa kitu uombezi wa waombezi. Yule mwenye kuyachinjia na kuyawekea nadhiri makaburi ni mshirikina na hautomfaa kitu uombezi.

Kwa kufupisha ni kwamba uombezi wenye kukanushwa, ni ule wenye kutafutwa pasi na idhini ya Allaah au kuombewa mshirikina. Ama kuhusu uombezi wenye kuthibitishwa, ni ule unaokuwa baada ya idhini ya Allaah na unakuwa kwa wale wenye kumuabudu Allaah peke yake.

[5] al-Bukhaariy (7510) na Muslim (193).

## 07. Msingi wa tatu

*Msingi wa tatu ni kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuja kwa watu waliokuwa ni wenye kutofautiana katika ´ibaadah zao. Miongoni mwao kuna ambao walikuwa wakiabudu Malaika, wengine walikuwa wakiwaabudu Mitume na waja wema, wengine wakiabudu mawe na miti na wengine wakiabudu mwezi na jua. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwapiga vita na hakutofautisha kati yao. Dalili ni maneno Yake (Ta´ala):*

وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الدِّينُ كُلُّهُ لِلَّهِ

***"Na piganeni nao mpaka kusiweko*** **fitnah** ***na Dini yote iwe kwa ajili ya Allaah." (08:39)***

**MAELEZO**

Msingi wa tatu ni kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitumwa kwa washirikina waliokuwa wakitofautiana katika ´ibaadah zao. Kuna ambao walikuwa wakiabudu Malaika, wengine wakiabudu jua na mwezi, wengine wakiabudu Mitume, masanamu, mawe na miti, na wengine wakiabudu mawalii na watu wema.

Kibaya cha ushirikina ni kuwa watu wake sio wenye kukubaliana juu ya kuabudu kitu kimoja, tofauti na wapwekeshaji ambao muabudiwa wao ni mmoja peke Yake (Subhaanahu wa Ta´ala):

أَأَرْبَابٌ مُّتَفَرِّقُونَ خَيْرٌ أَمِ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ مَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِهِ إِلَّا أَسْمَاءً سَمَّيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَآبَاؤُكُم

**"Je, waungu wengi wanaofarakana ni bora [kuabudiwa] au Allaah ambaye ni mmoja Pekee, mshindi? Hamuabudu pasi Naye isipokuwa majina mmeyaita nyinyi na baba zenu." (12:39-40)**

Katika ubatili wa shirki ni kuwa watu wake ni wenye kufarikiana katika ´ibaadah zao. Hili ni kwa sababu hawapiti juu ya msingi mmoja. Badala yake wanapita juu ya matamanio yao na madai ya wapotevu, kitu ambacho kinawafanya kufarikiana:

ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا رَّجُلًا فِيهِ شُرَكَاءُ مُتَشَاكِسُونَ وَرَجُلًا سَلَمًا لِّرَجُلٍ هَلْ يَسْتَوِيَانِ مَثَلًا ۚ الْحَمْدُ لِلَّهِ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ

**"Allaah amepiga mfano wa mtu aliyekuwa na washirika wagombanao na mtu mwengine aliyesalimika na bwana mmoja tu. Je, wanalingana sawa kwa hali zao? Himdi zote anastahiki Allaah! - bali wengi wao hawajui." (39:29)**

Ambaye anamuabudu Allaah peke yake ni kama mfano wa mtumwa ambaye anamilikiwa na bwana mmoja ambapo uwepo wake anaishi katika utulivu na amani. Anajua malengo na mahitajio yake na anaishi katika raha. Upande mwingine mshirikina ni kama mfano wa mtumwa anayemilikiwa na mabwana wengi na hajui ni yupi atamridhisha katika wao. Kila mmoja katika wao ana matamanio yake. Kila mmoja katika wao anataka kitu. Kila mmoja katika wao anataka amwendee yeye. Ndio maana amesema (Subhaanah):

ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا رَّجُلًا فِيهِ شُرَكَاءُ مُتَشَاكِسُونَ

**"Allaah amepiga mfano wa mtu aliyekuwa na washirika wagombanao... "**

Bi maana anamilikiwa na watu wengi na hajui ni yupi katika wao ambaye anatakiwa kumridhisha:

وَرَجُلًا سَلَمًا لِّرَجُلٍ

**"... na mtu mwengine aliyesalimika na bwana mmoja tu."**

Mtu huyu ana bwana mmoja anastarehe nae. Namna hii Allaah amepigia mfano kati ya mshirikina na ambaye anamuabudu Allaah peke yake.

Washirikina wanatofautiana katika ´ibaadah zao. Pamoja na hivyo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwapiga vita wote, pasi na kutofautisha

katika wao. Aliwapiga vita washirikina, mayahudi, manaswara, wenye kuabudu Malaika na waja wema, bila ya kutafautisha.

Hapa kuna Radd kwa wale wenye kusema:

"Ambaye analiabudu sanamu sio kama yule ambaye anamuabudu mja mwema au Malaika, kwa sababu watu hawa wa mwanzo wanaabudu mawe na miti vitu visivyokuwa na uhai. Ama kuhusu yule anayeabudu mtu mwema au walii, hazingatiwi ni kama ambaye anaabudu sanamu."

Kwa haya wanachotaka kusema ni kuwa yule anayeabudu makaburi hii leo anatofautiana na ambaye anaabudu masanamu na kwa ajili hiyo wanaonelea kuwa hakufuru na wala kitendo chake hichi hakizingatiwi kuwa ni shirki na hivyo hatimae haitojuzu kumpiga vita.

Tunasema: Mtume hakutofautisha kati yao, bali alionelea wote kuwa ni washirikina. Alihalalisha damu na mali yao, na wala hakufarikisha baina yao. Aliwapiga vita wale wanaomuabudu al-Masiyh ilihali al-Masiyh ni Mtume wa Allaah. Kadhalika aliwapiga vita mayahudi ambao wanamuabudu ´Uzayr ambaye ni mmoja katika Manabii wao au waja wema. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwapiga vita, hakutofautisha kati yao. Hakuna tofauti kati ya shirki kwa yule anayemuabudu mja mwema au sanamu, jiwe au mti, kwa sababu shirki ni kumtekelezea ´ibaadah asiyekuwa Allaah. Ndio maana anasema:

وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا

**"Na mwabuduni Allaah na wala msimshirikishe na chochote." (04:36)**

Neno "chochote" ni makatazo ya jumla yanayokusanya kila kitu anachoshirikishwa nacho Allaah (´Azza wa Jall), katika Malaika, Mitume, waja wema, mawalii, mawe na miti.

وَقَاتِلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الدِّينُ كُلُّهُ لِلَّهِ

**"Na piganeni nao mpaka kusiweko fitnah na Dini yote iwe kwa ajili ya Allaah." (08:39)**

Dalili ya kuwapiga vita washirikina pasi na kutofautisha kati yao vile wanavyoabudu ni maneno Yake (Ta´ala):

وَقَاتِلُوهُمْ

**"Na piganeni nao... "**

Hili ni jumla ya washirikina wote pasi na kubagua yeyote. Kisha akasema:

"

حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ

**"... mpaka kusiweko fitnah... "**

Neno "fitnah" yaani shirki na hivyo inakuwa na maana ya kwamba kusiwepo shirki. Sentesi imeenea na inagusa shirki aina zote, sawa iwe ni shirki na mawalii, watu wema, mawe, miti, jua au mwezi.

وَيَكُونَ الدِّينُ كُلُّهُ لِلَّهِ

**"... na Dini yote iwe kwa ajili ya Allaah."**

Bi maana ´ibaadah zote ziwe kwa ajili ya Allaah. Asishirikishwe na yeyote yule awae. Kwa hivyo hakuna tofauti kati ya shirki wanayofanyiwa mawalii, waja wema, mawe, miti, mashaytwaan au kitu kingine.

## 08. Kuna waliokuwa wakiabudu jua na mwezi

*Dalili ya jua na mwezi ni maneno Yake (Ta´ala):*

وَمِنْ آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ ۚ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ

***"Na katika ishara Zake, ni usiku na mchana na jua na mwezi. Basi msisujudie jua na wala mwezi; bali msujudieni Allaah Ambaye Aliyeviumba [hivyo] ikiwa Yeye Pekee mnawambudu." (41:37)***

**MAELEZO**

Ni dalili yenye kuonesha kuwa kuna watu wenye kusujudia jua na mwezi. Kwa ajili hii ndio maana Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekataza kuswali pindi jua linapochomoza na kuzama kwa ajili ya kufunga njia, kwa sababu kuna ambao wanalisujudia jua linapochomoza na linapozama. Kwa hivyo tumekatazwa kuswali katika nyakati hizi mbili hata kama swalah itakuwa kwa ajili ya Allaah. Maadamu kuswali katika nyakati hizi mbili kunakumbushia kitendo cha washirikina, ikakatazwa kwa ajili ya kufunga njia zote zinazopelekea katika shirki. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekuja kukataza shirki na kukataza vilevile njia zote zinazopelekea kwayo[6].

[6] Tazama "Fath-ul-Majiyd li Sharh Kitaab-it-Tawhiyd (02/835-839).

## 09. Kuna waliokuwa wakiwaaabudu Malaika na Mitume

*Dalili ya Malaika ni maneno Yake (Ta´ala):*

وَلَا يَأْمُرَكُمْ أَن تَتَّخِذُوا الْمَلَائِكَةَ وَالنَّبِيِّينَ أَرْبَابًا

***"Na wala hakuamuruni kuwafanya Malaika na Manabii kuwafanya miungu." (03:80)***

*Dalili ya Mitume ni maneno Yake (Ta´ala):*

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ أَأَنتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ إِلَٰهَيْنِ مِن دُونِ اللَّهِ ۖ قَالَ سُبْحَانَكَ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقٍّ ۚ إِن كُنتُ قُلْتُهُ فَقَدْ عَلِمْتَهُ ۚ تَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ ۚ إِنَّكَ أَنتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ

***"Na pale Allaah Atakaposema: "Ee 'Iysaa mwana wa Maryam! Je, wewe uliwaambia watu: "Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu miwili pasi na ya Allaah?" Atasema: "Utakasifu ni Wako! Hainipasi mimi kusema yasiyo kuwa haki kwangu; ikiwa nimesema hayo basi kwa yakini Ungeliyajua - Unayajua yale yote yaliyomo katika nafsi yangu na wala [mimi] sijui yale yaliyomo katika Nafsi Yako - hakika Wewe ni Mjuzi wa ghayb." (05:116)***

**MAELEZO**

Maneno Yake:

وَلَا يَأْمُرَكُمْ أَن تَتَّخِذُوا الْمَلَائِكَةَ

**"Na wala hakuamuruni kuwafanya Malaika... "**

ni dalili yenye kufahamisha kuwa kuna ambao wanaabudu Malaika na Mitume na kwamba hii ni shirki. Waabudu makaburi hii leo wanasema:

"Ambaye anawaabudu Malaika, Mitume na watu wema sio kafiri."

"Dalili ya Mitume... " hapa kuna dalili ´ibaadah wanayofanyiwa Mitume ni shirki kama ´ibaadah wanayofanyiwa masanamu.

Hapa kuna Radd kwa waabudu makaburi ambao wanatofautisha kati ya hayo mawili na kusema:

"Shirki ni kuabudu masanamu."

Hawalinganishi yule anayeabudu masanamu na ambaye anawaabudu mawalii na watu wema. Wanapinga ulinganisho huu na wanadai kuwa shirki ni kule kuyaabudu masanamu peke yake. Hili ni kosa la wazi kabisa kwa njia mbili:

1- Allaah (Jalla wa ´Alaa) amewakaripia wote katika Qur-aan na akaamrisha wapigwe vita.

2- Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakutofautisha kati ya wale wenye kuabudu masanamu, Malaika na waja wema.

## 10. Kuna waliokuwa wakiwaabudu waja wema

*Dalili ya waja wema ni maneno Yake (Ta´ala):*

أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ وَيَرْجُونَ رَحْمَتَهُ وَيَخَافُونَ عَذَابَهُ

***"Hao wanaowaomba [wao wenyewe] wanatafuta kwa Mola wao njia [na] kumkurubia kadri wanavyoweza, na wanataraji Rahmah Yake na wanakhofu Adhabu Yake." (17:57)***

**MAELEZO**

Hapa kunatajwa dalili yenye kuonesha kuwa kuna wenye kuabudu watu wema:

أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ

**"Hao wanaowaomba [wao wenyewe] wanatafuta kwa Mola wao njia [na] kumkurubia kadri wanavyoweza... "**

Aayah hii imeteremshwa kwa wale wenye kumuabudu al-Masiyh, mama yake na ´Uzayr. Ndipo (Subhaanah) akakhabarisha kuwa al-Masiyh, mama yake Maryam na ´Uzayr kwamba wote ni waja wa Allaah. Wanajaribu kujikurubisha kwa Allaah, wanatarajia huruma Wake na wanaogopa adhabu Yake. Wao wenyewe ni waja wanaomuhitajia Allaah, wanamuomba na wanatawassul Kwake kwa kumtii:

أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ

**"Hao wanaowaomba [wao wenyewe] wanatafuta kwa Mola wao njia [na] kumkurubia kadri wanavyoweza... "**

Bi maana kujikurubisha Kwake (Subhaanah) kwa kumtii na kumuabudu. Hii ina maana ya kwamba wao wenyewe ni wahitaji na mafukara wenye

kumuomba Allaah, wanatarajia huruma Wake na wanaogopa adhabu Yake, na kwa ajili hiyo hawastahiki kuabudiwa kwa kuwa ni wanaadamu.

Maoni mengine yanasema kuwa [Aayah hii] imeteremshwa kwa kundi la washirikina waliokuwa wakiyaabudu majini. Baada ya hapo majini haya yakasilimu na wale wenye kuwaabudu hawakutambua juu ya kusilimu kwao. Yakawa yanajikurubisha kwa Allaah, yanatarajia huruma Wake na kuchelea adhabu Yake. Kwa hivyo wao wenyewe ni wahitaji na mafukara wasiostahiki kuabudiwa.

Pasi na kujali malengo ya Aayah hii tukufu, inafahamisha kuwa haijuzu kuwaabudu waja wema. Ni mamoja wakawa ni Mitume, wakweli, mawalii au waja wema. Haijuzu kuwaabudu, kwa sababu wote ni waja mafukara wa Allaah, wenye kumuhitajia. Ni vipi basi wataabudiwa pamoja na Allaah (Jalla wa ´Alaa)?

Ukati kati/njia (*wasiylah*) maana yake ni utiifu na ukaribu. Kilugha maana yake ni "kitu chenye kufikisha katika malengo". Kitu chenye kufikisha katika radhi na mapenzi ya Allaah ni njia ya kumwendea. Huu ndio ukati kati uliowekwa kwenye Shari´ah katika maneno Yake (Ta´ala):

وَابْتَغُوا إِلَيْهِ الْوَسِيلَةَ

**"Tafuteni Kwake njia." (05:35)**

Ama kuhusu waliopinda na wapumbavu wanasema:

"Ukati kati ni kuweka baina yako wewe na Allaah mawalii, watu wema au maiti ili wakukurubishe kwa Allaah."

مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ

**"Hatuwaabudu isipokuwa kwa lengo la kutukurubisha kwa Allaah**

**ukaribu." (39:03)**

Hivi ndivyo wanavyofasiri "ukati kati/njia" wapumbavu hawa. Wanaonelea kuwa unatakiwa kuweka mkati kati baina yako wewe na Allaah anayekutambulisha kwa Allaah, kukufikishia mahitajio yako na kuelezea juu yako. Ni kana kwamba Allaah (Jalla wa ´Alaa) Mwenyewe hajui au ni bakhili ambaye hatoi isipokuwa baada ya kuombea Kwake - ametakasika Allaah (Jalla wa ´Alaa) na yale wanayoyasema! Wanawapaka watu mchanga wa machoni na kuwaambia kuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa) anasema:

أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ

**"Hao wanaowaomba [wao wenyewe] wanatafuta kwa Mola wao njia ya kujikurubisha kwa Allaah... "**

Wanasema kuwa hii ni dalili inayoonesha kuwa kuweka wakati kati mbele ya Allaah katika viumbe ni kitu kimewekwa katika Shari´ah kwa sababu Allaah amewasifia wale wenye kufanya hivo. Katika Aayah nyingine imekuja:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَابْتَغُوا إِلَيْهِ الْوَسِيلَةَ

**"Enyi mlioamini! Mcheni Allaah na tafuteni Kwake njia." (05:35)**

Hapa wanasema:

"Allaah ametuamrisha kufanya ukati kati wa kumfikia na ukati kati huu maana yake ni kuweka wakati kati."

Namna hii ndivyo wanayapotosha maneno kuyaondosha mahala pake stahiki.

Ukati kati uliowekwa katika Qur-aan na Sunanh ni utiifu unaokurubisha kwa Allaah, kwa kufanya Tawassul kwa majina na sifa Zake (Subhaanahu wa Ta´ala). Huu ndio ukati kati uliyowekwa katika Shari´ah.

Kuhusu kufanya Tawassul kwa Allaah kupitia viumbe, ni jambo limekatazwa na ni ukati kati wa kishirki, nao ndio uliyofanywa na washirikina hapo kale:

وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَٰؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِندَ اللَّهِ

**"Na wanaabudu asiyekuwa Allaah ambao [hawawezi] kuwadhuru na wala kuwanufaisha na wanasema: “Hawa ni waombezi wetu mbele ya Allaah."" (10:18)**

وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ إِنَّ اللَّهَ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ فِي مَا هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ كَاذِبٌ كَفَّارٌ

**"Na wale wanaowafanya wengine badala Yake kuwa walinzi [wakisema]: “Hatuwaabudu isipokuwa kwa lengo la kutukurubisha kwa Allaah ukaribu.” Hakika Allaah Atahukumu baina yao katika yale yote waliyokhitilafiana nayo. Hakika Allaah Hamwongoi aliye muongo, kafiri." (39:03)**

Hii ndio shirki ile ile ya watu wa kale na waliokuja nyuma. Hata kama wataita kuwa ni "ukati kati" si jengine isipokuwa ni shirki na sio ukati kati aliyouweka Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Allaah kamwe hakufanya shirki iwe ni njia ya kumfikia. Badala yake ni kuwa shirki inamuweka mtu mbali kabisa na Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala):

إِنَّهُ مَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ

**"Hakika mwenye kumshirikisha Allaah bila shaka Allaah atamharamishia Pepo." (05:72)**

Ni vipi basi shirki itakuwa ni njia ya kumfikia Allaah? Allaah ametakasika na yale wanayoyasema!

Kinacholengwa katika Aayah ni kwamba inafahamisha kuwa kuna washirikina wenye kuwaabudu watu wema. Allaah amebainisha hilo, na kwamba wale wanaowaabudu ni waja wahitaji na kwamba:

يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ

**"... wanatafuta kwa Mola wao njia [na] kumkurubia...**

Bi maana wanajikurubisha Kwake kwa kumtii:

أَيُّهُمْ أَقْرَبُ

**".. kadri wanavyoweza... "**

Bi maana wanashindana kwa ajili ya Allaah (Jalla wa ´Alaa) kupitia ´ibaadah kwa sababu wanamuhitajia Allaah:

وَيَرْجُونَ رَحْمَتَهُ وَيَخَافُونَ عَذَابَهُ

**"... na wanataraji Rahmah Yake na wanakhofu Adhabu Yake... " (17:57)**

Ambaye hali yake imeshakuwa namna hii hastahiki kuwa mungu, anayeombwa na kuabudiwa pamoja na Allaah (´Azza wa Jall).

## 11. Kuna waliokuwa wakiabudu mawe na miti

*Dalili ya miti na mawe ni maneno Yake (Ta´ala):*

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ وَمَنَاةَ الثَّالِثَةَ الْأُخْرَىٰ

***"Je, mmeona al-Laat na al-'Uzzaa? Na Manaat mwengine wa tatu?" (53:19-20)***

**MAELEZO**

Aayah hii inathibitisha kwamba kuna washirikina wenye kuabudu mawe na miti.

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ

**"Je, mmeona al-Laat... "**

ni swali la kukemea, likiwa na maana "Nijuzeni", kwa njia ya swali la kukemea na kutweza.

"al-Laat" ilikuwa ni sanamu at-Twaaif ambalo lilikuwa ni jiwe lililozikwa. Ilikuwa ni jengo liliyojengwa sawa na Ka´bah. Ilikuwa limezungukwa na uwanja ulio na walinzi. Walikuwa wakiliabudu badala ya Allaah (´Azza wa Jall). Lilikuwa la Thaqiyf na washirika wao katika makabila mbalimbali ambao walikuwa wakijifakharisha nalo.

al-Laat alikuwa ni mwanaume mwema aliyekuwa akipika uji na akiwapa mahujaji. Alipokufa, akajenga jengo juu ya kaburi lake ambalo walilifunika kwa pazia. Hivyo wakawa wanaliabudu badala ya Allaah (´Azza wa Jall).

"al-´Uzzaa... " ilikuwa ni miti mingi ya mtende kati ya Makkah na at-Twaaif. Pembezoni mwake kulikuwa jengo lililofunikwa likiwa na walinzi. Kulikuwa mashaytwaan yanayozungumza na watu. Wajinga walikuwa wakidhania

kwamba miti na jengo vyenyewe ndivyo vinavyozungumza na wao. Ilikuwa ni mashaytwaan ndio wenye kuzungumza nao ili kuwapoteza na njia ya Allaah. Sanamu hili lilikuwa la Quraysh, watu wa Makka na walioko pembezoni mwake.

"Manaat... " ilikuwa ni jiwe kubwa lililokuwa karibu na mlima wa Qudayd kati ya Makkah na al-Madiynah. Lilikuwa ni la Khuzaa´ah, al-Aws na al-Khazraj. Walikuwa wakihirimia kutoka kwenye jiwe hilo wanapoelekea hajj na wanaliabudu badala ya Allaah.

Haya ndio yalikuwa masanamu matatu makubwa ya waarabu.

Allaah (Ta´ala) anasema:

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ وَمَنَاةَ الثَّالِثَةَ الْأُخْرَىٰ

**"Je, mmeona al-Laat na al-'Uzzaa? Na Manaat mwengine wa tatu?"**

Je, yalikupeni faida yooyte? Yalikunufaisheni? Yalikuwa yakikunusuruni? Je, yalikuwa yakiumba, yakiruzuku, yakihuisha na yakifisha? Mlipata nini kwayo? Hili ni kwa njia ya kukemea na kuzizindua akili ziweze kurudi katika usawa wake. Vitu hivi si vyengine isipokuwa ni mawe na miti isiyonufaisha wala kudhuru.

Pindi Allaah alipoleta Uislamu na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akaiteka Makkah, alimtuma al-Mughiyrah bin Shu´bah na Abu Sufyaan bin Harb kuliendea al-Laat katika mji wa at-Twaaif na akawaamrisha waliangamize. Kadhalika akamtuma Khaalid bin al-Waliyd kuliendea al-´Uzzaa na akaliharibu, akaukata mti na akaliua jini la kike lililokuwa likizungumza na watu ili kuwapoteza - himdi zote ni za Allaah. Vilevile akamtuma ´Aliy bin Abiy Twaalib kuliendea Manaat akaliharibu na kulitokomeza[7].

[7] Tazama "Zaad-il-Ma´aad" (04/413-415).

Ikiwa masanamu haya yalishindwa kujiokoa yenyewe, ni vipi yangeliweza kuwaokoa watu wake na wale wenye kuyaabudu?

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ وَمَنَاةَ الثَّالِثَةَ الْأُخْرَىٰ

**"Je, mmeona al-Laat na al-'Uzzaa? Na Manaat mwengine wa tatu?"**

Yalienda wapi? Yalikunufaisheni? Je, yaliweza kujitetea kutokamana na maaskari wa Allaah na majeshi ya wapwekeshaji?

Hii ni dalili yenye kuthibitisha kwamba kuna watu wenye kuabudu miti na mawe. Masanamu haya matatu ndio yalikuwa makubwa lakini pamoja na hivyo Allaah alitokomeza uwepo wake. Hayakuweza kujitetea yenyewe na wala hayakuweza kuwanufaisha watu wake. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwapiga vita pasi na kuzuiwa na masanamu yao. Haya ndiyo yaliyotajwa na Shaykh (Rahimahu Allaah) ili kuthibitisha kuwa kuna ambao walikuwa wakiabudu mawe na miti.

Ametakasika Allaah! Ni vipi watu wenye busara wanaweza kuabudu miti na mawe vitu visivyokuwa na uhai, akili na wala havifanyi harakati? Iko wapi akili ya mwanaadamu? Ametakasika Allaah na yale wanayoyasema!

## 12. Ukhatari wa kuwa na ujinga juu ya Tawhiyd

*Abu Waaqid al-Laythiyy (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:*

*"Tulitoka pamoja na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwenda Hunayn na sisi ndio punde tu tumetoka katika ukafiri. Washirikina walikuwa na mkunazi unaoitwa "Dhaat Anwaatw" wakiuadhimisha na kutundika silaha zao. Tukapita karibu na mkunazi huo tukasema: "Ee Mtume wa Allaah, tufanyie Dhaat Anwaatw kama jinsi na wao walivyokuwa na Dhaat Anwaatw. Ndipo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Subhaan Allaah! Haya ndio yale yale yaliyosemwa na watu wa Muusa: "Tufanyie mungu kama jinsi na wao walivyokuwa na mungu." Ninaapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake; mtafuata desturi za waliokuwa kabla yenu.""*[8]

**MAELEZO**

Abu Waaqid al-Laythiy (Radhiya Allaahu ´anh) alikuwa ni mmoja katika wale waliosilimu mwaka wa Ushindi wa nane baada ya Kuhajiri.

"Anwaatw" ni wingi wa "Nawt" ikiwa na maana ya kutundika. Walikuwa wakitundika silaha zao kwa ajili ya kutafuta baraka. Haya yalisemwa na Maswahabah ambao wamesilimu karibuni na bado hawajaielewa Tawhiyd sawa sawa.

"... tufanyie Dhaat Anwaatw kama jinsi na wao walivyokuwa na Dhaat Anwaatw... " hili ndio mtihani wa kufuata kichwa mchunga na kuiga. Huu ndio mtihani mkubwa. Hapo ndipo alistaajabu Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kweli kweli na akasema:

"Allaahu Akbar! Allaahu Akbar! Allaahu Akbar!"

[8] at-Tirmidhiy (2180), Ahmad (05/218), Ibn Abiy ´Aaswim (76) na Ibn Hibbaan (6702). Ni Swahiyh kwa mujibu wa Ibn Hajar katika "al-Iswaabah" (04/216).

Alikuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anaposhangazwa na kitu au anapokemea jambo, alikuwa akisema kwa kukariri aidha "Allaahu Akbar" au "Subhaan Allaah".

"... mtafuata desturi za waliokuwa kabla yenu."

Bi maana njia wanazopita juu yake watu na baadhi kuwaiga wengine. Hakuna kilichowafanya kusema haya isipokuwa kuwafuata wa kale na kujifananisha na washirikina.

"Haya ndio yale yale yaliyosemwa na watu wa Muusa: "Tufanyie mungu kama jinsi na wao walivyokuwa na mungu."

Baada ya Muusa (´alayhis-Salaam) kuvuka bahari na wana wa israaiyl na Allaah akamzamisha adui yao ilihali wanashuhudia, waliwapitia watu waliokuwa wakiyaadhimisha masanamu yao. Watu hawa wakamwambia Muusa:

اجْعَل لَّنَا إِلَٰهًا كَمَا لَهُمْ آلِهَةٌ ۚ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُونَ

**"Hebu tufanyie na sisi mungu kama hawa walivyokuwa na miungu. [Muusa] akasema: "Hakika nyinyi ni watu mnaofanya ujahili.""**

Akawakemea na kuwaambia:

إِنَّ هَٰؤُلَاءِ مُتَبَّرٌ مَّا هُمْ فِيهِ

**"Hakika hawa yatateketezwa yale waliyo nayo... "**

Bi maana batili:

وَبَاطِلٌ مَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ

**"... na ni yenye kubatilika yale waliyokuwa wakiyatenda." (07:138-139)**

Kwa sababu kitendo ni cha shirki:

أَغَيْرَ اللَّهِ أَبْغِيكُمْ إِلَٰهًا وَهُوَ فَضَّلَكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ

**"Je, nikutafutieni mungu asiyekuwa Allaah na hali Yeye amekufadhilisheni juu ya walimwengu?" (07:140)**

Akawakemea (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) kama ambavyo Mtume wetu (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwakemea watu hawa. Lakini pamoja na hivyo watu hawa hawakushirikisha. Wana wa israaiyl hawakufanya shirki, kwa sababu hawakufanya jambo hilo. Kadhalika Maswahabah; lau wangechukua Dhaat Anwaatw wangelikuwa wametumbukia katika shirki. Lakini Allaah akawakinga. Pindi Mtume wao alipowakataza, wakajiepusha. Walisema maneno haya kwa sababu ya ujinga, na si kwa kukusudia. Pindi walipotambua kuwa kitendo hicho ni shirki, wakakomeka na hawakufanya kitu.

Kikusudiwacho katika Aayah ni kwamba kuna ambao wanaabudu miti. Washirikina hawa walichukua Dhaat Anwaatw na vivyo hivyo Maswahabah hawa kutokana na uchache wa elimu walijaribu kujifananisha na washirikina, lakini Allaah akawa amewalinda kwa Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Kinacholengwa ni kuwa kuko ambao wanatafuta baraka kupitia miti na kuiadhimisha. Kuiadhimisha maana yake ni kubaki karibu nayo kwa muda mrefu kwa ajili ya kujikurubisha kwayo. Uadhimisho ni kubaki sehemu.

Hapa kunapata kubainika mambo mengi makubwa:

**La kwanza:** Ukhatari wa kuwa na ujinga juu ya Tawhiyd. Ambaye ni mjinga juu ya Tawhiyd ni vyepesi kwake kutumbukia katika shirki. Kuanzia hapa ni wajibu kujifunza Tawhiyd na kujifunza yenye kupingana nayo, ambayo ni shirki, ili mtu aweze kuwa juu ya yakini na ujuzi. Hili khawsa pale ambapo mtu atamuona mwenye kufanya hivo na huku akidhania kuwa ni haki kwa sababu ya ujinga. Hapa kuna ukhatari wa ujinga, na khaswa kuhusiana na ´Aqiydah.

**La pili:** Katika Hadiyth kuna ukhatari wa kujifananisha na washirikina. Kujifananisha huku kunaweza kupelekea katika shirki. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Mwenye kujifananisha na watu, basi yeye ni katika wao."**[9]

Hivyo haijuzu kujifananisha na washirikina.

**La tatu:** Ni shirki kutafuta baraka kupitia mawe, miti na majengo. Haijalishi kitu hata kama mwenye kufanya hivo atayapa majina mengine. Kutafuta baraka kutoka kwa mwengine asiyekuwa Allaah katika mawe, miti, makaburi na mawalii ni shirki

[9] Abu Daawuud (4031) na Ahmad (02/50). Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah amesema: "Mnyororo wake ni mzuri." (Iqtidhwaa´ as-Swiraatw al-Mustaqiym (01/236-239)). Haafidhw al-´Iraaqiy amesema: "Mlolongo wa wapokezi wake ni Swahiyh." (Taariykh-ul-Ihyaa' (02/65)). Haafidhw bin Hajar amesema: "Mlolongo wa wapokezi wake ni mzuri." (Fath-ul-Baariy (06/98)).

## 13. Msingi wa nne

*Msingi wa nne: washirikina wa zama zetu ushirikina wao ni wa khatari zaidi kuliko washirikina wa mwanzoni. Washirikina wa mwanzoni walikuwa wakifanya shirki katika kipindi cha raha, wakati katika kipindi cha shida walikuwa ni watakasifu katika ´ibaadah. Ama washirikina wa zama hizi ni wenye kufanya shirki katika kipindi chote, sawa iwe ni wakati wa raha au shida.*

**MAELEZO**

Msingi wa nne na ndio wa mwisho ni kuwa washirikina wa leo ushirikina wao ni wa khatari zaidi kuliko washirikina wale ambao Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitumwa kwao.

Sababu ya hilo iko wazi. Allaah (Jalla wa ´Alaa) ameeleza kuwa washirikina wa kale walikuwa wakimtakasia ´ibaadah Allaah pindi wanapofikwa na matatizo. Walikuwa hawamuombi mwengine asiyekuwa Allaah (´Azza wa Jall) kwa sababu walitambua kuwa hakuna yeyote anayeokoa kutoka katika matatizo isipokuwa Allaah (´Azza wa Jall). Amesema (Ta´ala):

فَإِذَا رَكِبُوا فِي الْفُلْكِ دَعَوُا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ فَلَمَّا نَجَّاهُمْ إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ

**"Wanapopanda merikebu [wakakumbwa na misukosuko] humwomba Allaah kwa kumtakasia Yeye Dini; lakini Anapowaokoa [kwa kuwafikisha salama] nchi kavu, tahamaki hao wanamshirikisha." (29:65)**

وَإِذَا غَشِيَهُم مَّوْجٌ كَالظُّلَلِ دَعَوُا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

**"Na yanapowafunika mawimbi kama vivuli humwomba Allaah hali ya kumtakasia Yeye Dini." (31:32)**

Bi maana wanamuomba.

فَلَمَّا نَجَّاهُمْ إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ

**"Lakini Anapowaokoa katika nchi kavu, tahamaki hao wanamshirikisha." (29:65)**

Washirikina wa kale walikuwa wakishirikisha kwa kuyaomba masanamu, miti na mawe katika kipindi cha raha. Ama wanapofikwa na matatizo na wanayaona maangamivu mbele yao, basi wanamuomba Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) peke yake, na wanayasahau masanamu, miti, mawe na viumbe wengine wote. Ni vipi mtu atamuomba mwengine asiyekuwa Allaah wakati wa raha ikiwa hakuna anayeokoa kutoka katika matatizo isipokuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa) peke yake?

"Washirikina wa zama zetu" bi maana watu waliokuja nyuma katika Ummah wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) waliotumbukia katika shirki. Shirki zao zinakuwa wakati wote sawa katika raha na shida. Hawamuabudu Allaah hata katika kipindi cha matatizo. Bali kila wanapofikwa na matatizo, ndivyo jinsi shirki zao zinavyoongezeka na kumuomba al-Hasan, al-Husayn, ´Abdul-Qaadir, ar-Rafaa´iy na wengineo. Hili ni jambo linalojulikana. Wananasibishiwa vituko mbalimbali vinavyotokea huko baharibini. Pindi mambo yanapowawia mazito huita majina ya mawalii na watu wema na wanawaomba ulinzi na msaada badala ya Allaah (´Azza wa Jall). Hili ni kwa sababu walinganizi wa batili na wa upotevu wanawaambia:

"Tutakuokoeni kutokana na bahari. Mkifikwa na kitu basi iteni majina yetu na sisi tutakuokoeni."

Haya yanapokelewa kutoka kwa wasomi wa Suufiyyah. Mnaweza kusoma "Twabaqaat ash-Sha´raaniy". Humo mna mambo yanayoifanya ngozi kusisimka pindi mtu anaposoma karama za mawalii; wanawaokoa watu kutokamana na mawimbi na wananyoosha mikono yao kwenye bahari na wanabeba boti lote mpaka wanawafikisha nchikavu bila ya mikono yao kulowa. Haya ni baadhi tu ya uongo na ukhurafi wao. Pamoja na kuwa shirki

zao ni wakati wote wa raha na shida, ni mbaya zaidi kuliko za washirikina wa kale.

Vilevile imetangulia kusema Shaykh katika "Kashf-ush-Shubuhaat"[10]:

"Watu wa mwanzo walikuwa wakiabudu watu wema katika Mitume, Manabii na mawalii, na ama watu hawa wanawaabudu watenda madhambi ambao wao wenyewe wanalikubali hilo. Wale wanaowaita kuwa ni mabwana na waokozi hawaswali, hawafungi na hawajitengi mbali na uzinzi, liwati na madhambi mengine. Wanaonelea kuwa ´ibaadah haiwawajibikii tena. Ya halali na ya haramu hayatumiki tena kwao, bali ni kwa wasiokuwa wasomi peke yao. Wao wenyewe wanakubali kuwa mabwana wao hawaswali, hawafungi na hawajiepushi na madhambi. Pamoja na hivyo wanawaabudu. Bali wanawaabudu watu ambao ni waovu kabisa. Mfano wa hao ni al-Hallaaj, Ibn ´Arabiy, ar-Rifaa´iy, al-Badawiy na wengineo."

[10] Tazama "Kashf-ush-Shubuhaat", uk. 169-170, katika "Mu´allafaat al-Imaam al-Mujaddid", kitengo cha ´Aqiydah.

## 14. Hitimisho

*Dalili ni maneno Yake (Ta´ala):*

فَإِذَا رَكِبُوا فِي الْفُلْكِ دَعَوُا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ فَلَمَّا نَجَّاهُمْ إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ

***"Wanapopanda merikebu [wakakumbwa na misukosuko] humwomba Allaah kwa kumtakasia Yeye Dini; lakini Anapowaokoa [kwa kuwafikisha salama] nchi kavu, tahamaki hao wanamshirikisha." (29:65)***

**MAELEZO**

Shaykh ametaja dalili kuonyesha kuwa washirikina waliokuja nyuma wana shirki kubwa na ya khatari kuliko washirikina wa kale, kwa sababu washirikina wa kale walikuwa wakimtakasia ´ibaadah Allaah katika kipindi cha shida na wakimshirikisha wakati wa raha. Amesema (Ta´ala):

فَإِذَا رَكِبُوا فِي الْفُلْكِ دَعَوُا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

**"Wanapopanda merikebu [wakakumbwa na misukosuko] humwomba Allaah kwa kumtakasia Yeye Dini."**

Swalah na salaam zimwendee Mtume wetu Muhammad, kizazi chake na Maswahabah zake.